



Zanzibar,

21 Januari, 2023

**RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi amewataka wahitimu wa vyo vikiu nchini kujikita kwenye utafiti utakaotoa ufumbuzi wa matatizo yaliyomo kwenye jamii.**

Aidha, alivitaka vyo vikiu kuongeza program kwa mujibu wa mahitaji ya wakati uliopo na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia duniani ili kuleta mabadiliko nchini

Dkt. Mwinyi alitoka kauli hizo kwenye Mahafali ya 22 ya Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al-Sumait, Chukwani Wilaya ya Magharibi B, Unguja.

Aliwataka wahitimu wa chuo hicho kutumia utafiti wao kwa lengo la kutatua changamoto zilizomo kwenye jamii badala kuuweka kwenye maktaba na kuufungia.

Rais Dk. Mwinyi alizishauri Wizara na Idara za Serikali kushirikiana na vyo vikiu kufanya utafiti wenye kuchochea maendeleo kwenye nyanja zote za jamii, uchumi, tehamu na mawasiliano ili kuleta mabadiliko yenye tija. Aliwasihahi wahitimu watakabahatika kuajiriwa ama kujajiri baada ya kuhitimu mafunzo yao, wakafanyekazi kwa uadilifu, kujituma na kuchunga maadili mema yanayokubalika katika jamii ili kuleta mabadiliko kwenye utendaji wao.

Aidha, aliwataka wakawe wabunifu wa kuzitafuta fursa za kujiendeleza zaidi na kuzitumia kwa weledi na ufanisi wa hali ya juu kwa lengo la kujiimarisha kitaaluma. Hata hivyo, aliwaasa wanafunzi wanaoendelea na masomo chuoni hapo kuendelea kudumisha nidhamu na kufuata mazuri ya watangulizi wao kwa kuwa na maadili mema ya kutafuta elimu ili wapate ufaulu mzuri

Akizungumza kwenye mahafali hayo, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhamed Mussa aliwataka wahadhiri wa chuo hicho kujikita zaidi kwenye kutoa elimu ya ufundi na mafunzo ya amali kwa kuwapa uwezo wanafunzi wakujajiri wanapokamilisha masomo yao.

Alisema Sera ya elimu inawataka wanafunzi watakapomaliza masomo yao yalazima kwa ngazi ya sekondari, kuwe na sehemu ya wao kupata kujiendeleza kwa ustadi na ufundi.

Chuo cha Abdulrahman Al Sumait chini ya uongozi wa Mkuu wake, Dk. Aman Abeid Karume, Rais Mstaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar awamu ya sita, kina jumla ya wanafunzi 4553 tokea kuanzishwa kwake mwaka 1998. Jumla ya wanafunzi 310 wakiwemo wanawake 183 na wanaume 127 walihitimu kwenye mahafali hayo.

  
Charles Hilary  
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

